

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", GEITA
Namba ya Simu: +255 759 – 695972
Barua pepe. hospital@geitarrh.go.tz
(Barua zote ziandikwe kwa (Mganga Mfawidhi)



Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,
77 Barabara ya Simon Sirro
S.L.P. 40,
30150 BOMBAMBILI GEITA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na.AB.165/307/01 C/80

01.04.2026

Wananchi wote,
TANZANIA

Kuh: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA AJIRA YA MKATABA WA KUJITOLEA

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita anawatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi mbalimbali za kazi kwa Mkataba kwa muda wa mwaka mmoja. Nafasi husika ni kama ifuatavyo; -

1.0 MTAALAMU WA USINGIZI NA GANZI (ANESTHETIST) – NAFASI 3

1.1 Sifa za Mwombaji:

Mwenye Astashahada ya Usingizi na Ganzi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali

1.2 Majukumu yake:

- a) Kutoa Huduma za Usingizi (Anesthesia) Wakati wa Upasuaji;
- b) Kufanya Tathmini ya Wagonjwa Kabla ya Upasuaji (Pre-operative Assessment)
- c) Kufuatilia na Kusimamia Hali ya Mgonjwa Wakati wa Upasuaji;
- d) Kujua aina ya upasuaji unaenda kufanyika
- e) Kusimamia huduma baada ya upasuaji (Post-operative Care).
- f) Kusimamia Maumivu (Pain Management) baada ya upasuaji, kwa wenye magonjwa sugu na Katika huduma za dharura
- g) Kushiriki Katika Huduma za Dharura za wagonjwa mahututi, Uokoaji wa maisha (resuscitation) na huduma za ajali na dharura
- h) Kusimamia Vifaa vya Anesthesia na Oxygen katika kusimamia mashine za anesthesia, Kusimamia upatikanaji wa oksijeni na kuhakikisha vifaa vinafanya kazi vizuri
- i) Kuhakikisha Usalama wa Wagonjwa wanazingatia Miongozo ya usalama wa upasuaji, Matumizi sahihi ya dawa na Kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza.
- j) Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:

- 1. Ngazi ya mshahara ya kila nafasi itazingatia Mwongozo wa Kitaifa uliotolewa Jula 2025** unaohusu namna ya kushughulikia Watumishi wa kujitolea katika Utumishi wa Umma;
- Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
- Kila mwaombaji anatakiwa aambatishe nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na taaluma vinavyohitajika kulingana na Kada husika kama ilivyofafanuliwa katika tangazo hili;
- Kila Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa;
- Uwasilishaji wa vyeti vya kugushi utapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria;**
- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) akionesha namba za simu na anuani yake kwake na za wadhamini watatu (3) wa uhakika.
- Mwombaji aambatishe picha ndogo (Passport size) mbili (2) kwenye barua ya maombi;
- Mwombaji awe tayari kupangwa na kubadilishiwa eneo la kazi kadri ya mahitaji ya mwajiri.
- Mwombaji awe nadhifu na nidhamu ya hali ya juu.
- Waombaji ambao kada zao zinawahitaji wasajiliwe na Bodi zao za taaluma waambatanishe vyeti vya usajiri na Leseni hai kwa kada ambazo hupewa leseni
- Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili na watakaoshindwa kuzingatia masharti ya Tangazo hili hawataitwa;
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **14.04.2026**
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya **Posta** kwa anuani ifuatayo: -

**Mganga Mfawidhi,
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita,
S.L.P 40,
GEITA**

metolewa na: -

Dkt. Fatuma Juma Sitta
**MGANGA MFAWIDHI,
HOSPITALI YA RUFEE YA MKOA WA GEITA.**